**SHULE YA SEKONDARI THEMI HILL**
**MASWALI YA KISWAHILI APR-JUNI,2020.**
**KISWAHILI, KIDATO CHA TATU.**

- **UFAHAMU.**

**Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.**

Itakumbukwa kuwa mwaka wa 1964 ulifikisha Taifa letu mwisho wa mpango wake wa maendeleo ya miaka mitatu. Lakini kama tunavyojua mwaka huohuo ulitufunulia sura mpya katika historia ya Taifa letu. Yaani mwanzo wa mipango wetu mashuhuri ya maendeleo ya miaka mitano. Hatua mahususi zilizochukuliwa mpaka sasa tangu kuanzishwa kwa mpango huo zimeonekana hasa katika mwaka huu wa 1965. Kwa hiyo tutakubali kuwa huu ulikuwa mwaka wa maana katika jitihada ya Taifa letu katika kutekeleza mpango huo, serikali ilitaja mambo mengi ya lazima kwa kufanikisha mipango. Tatizo kubwa lililozuka katika mwaka huu wa kwanza ni uhaba wa wataalamu pamoja na fedha, fedha za kuendeshes mpango huu maalumu. Bila shaka hii ni shida kubwa kwani haikuwa kama ilivyotarajiwa.

Imejuzu migogo katika makisio ya mpango huo. Wataaluma kama mia tano (500) hivi walikisiwa na serikali yetu kutoka nchi za kigeni. Twaweza kufahamu ni gharama kubwa inayohitajiwa katika jambo hili kwa vyovyote vile serikali haikuweza kuleta wataalamu wote jinsi ilivyotakiwa na shuruti za mafanikio ya mpango wa maendeleo. Sababu mbalimbali ziliungana kutia ugumu katika tatizo la kupata wataalamu. Serikali ilijitahidi kuleta wataalamu wa kutosha. Ubovu mwingine ulizidi kutoleta maendeleo ni ukosefu wa wafanyakazi wa zile kazi zilizoachwa na wale walioacha kazi au waliomaliza mikataba ya kazi. Wengi katika hao utumishi wao ulihitajiwa na Taifa hili. Hivyo kuacha kazi kwa wageni hao kulizidi kupanua pengo la shida ya kupata wataalamu wa kutosha kutoka nchi za nje. Wakati huohuo serikali

Ilitia jitihada ili kuwapata wataalamu ambao ni wana wa Taifa hili kwa kuwapa elimu na ujuzi wa juu ili mnamo mwaka wa 1968, Tanzania iweze kuwa na hesabu kubwa zaidi ya wajuzi wanaotakiwa. Hii ni njia njema na fahari ya baadaye; lakini vilevile ni lazima ikubaliwe kuwa jitihada na uwezo wa serikali au Taifa lenyewe, haitoshelezi haja inayokabili Tanzania kwa siku hizi.

Ni rahisi kuacha kuwapa wana wa Tanzania taaluma ya wataalamu ili gharama ambayo ingetumiwa kwa kazi hiyo ipelekwe na kuungwa kwa ile inayotakiwa kwa kuweza kuwapata wataalamu hao wote 500, Bali wafikiri mpaka lini Tanzania itategemea wataalamu wa kigeni?

Je ni fahari kwa Taifa lolote huru kubaki nyuma katika haja ya kujitosheleza

**Maswali:**

1. Kichwa cha habari kinachoweza kufaa habari hii ni kipi?
2. Taja matatizo mawili yaliyoikabili serikali ya Tanzania mwanzoni mwa mpango wa miaka mitano.
3. Taja nomino tano zilizotajwa katika habari uliyosoma.
4. Ni mwaka gani ulikuwa wa maana kwa mipango ya maendeleo yaTaifa kwa miaka mitano?
5. Habari hiyo ina aya ngapi?
6. Fupisha habari uliyosoma kwa maneno yasiyopungua hamsini (50).

**Fafanua dhana ya Istilahi zifuatazo kisha toa mfano mmoja kwa kila dhana uliyofafanua**.

7. Lugha
8. Lugha Fasaha
9. Lugha isiyo fasaha
10. Kamusi
11. Kidahizo

**Eleza maana ya vidahizo vifuatavyo:**

12. Kinyenyezi
13. Matandu
14. Matlaba
15. Sandali
16. uzimbezimbe
17. Kitomeo
18. Shamirisho
19. Chagizo
20. Prediketa
21. Irabu
22. Konsonanti
23. Kirai
24. Kiima
25. Kiarifu
26. Prediketa
27. Kirai Nomino
28. Kirai Kivumishi
29. Kitai Kiunganishi
30. Kirai Kitenzi
31. Kirai Kiunganishi
32. Kirai Kielezi
33. Rejesta ni nini?

**Eleza kwa mifano kuonesha rejesta inayotumika katika sehemu zifuatazo:**

34. Hotelini
35. Mahakamani
36. Sokoni
37. shuleni
38. Hospitalini
39. Ndani ya mabasi

**Istilahi moja inaweza ikawa na majina mawili. Andika majina mengine ya dhana zifuatazo:**

40. Chagizo
41. Shamirisho
42. Prediketa
43. Kuainisha
44. Mofimu za wakati
45. Tungo ni nini?
46. Tungo Neno ni nini?
47. Tungo Kirai ni nini?

48. Tungo Kishazi ni nini?
49. Tungo Sentensi ni nini?
50. Eleza maana ya ngeli za Nomino.
51. Kwa kutumia kigezo cha Upatanisho wa kisarufi,taja ngeli tisa (9) za nomino.
52. Taja aina kuu nne za tungo katika lugha ya Kiswahili.
53. Eleza maana ya sentensi,kisha taja aina kuu za sentensi katika lugha ya Kiswahili.
54. Fafanua aina kuu za sentensi katika lugha ya Kiswahili.
55. Eleza maana ya uchanganuzi wa sentensi,
56. Taja njia kuu zitumikazo katika uchanganuzi wa sentensi.
57. Fafanua hatua kuu za kuzingatia katika uchanganuzi wa sentensi.

**Tungo zifuatazo ni tata, eleza maana ya utata kisha toa maana mbili kwa kila tungo;-**

58. Ali anampenda dada yangu.
59. Nyumba ile ni ya wageni.
60. Jordan ana ua nyumbani kwake.
61. Atakuja jumanne.
62. Mwalimu ameacha kazi
63. Kaka ana nyanya.
64. Jana tuliona paa.
65. Mama anafurahia pango
66. Mwalimu anafundisha barabara
67. Alimpigia ngoma
68. Kijana amepata fomu
69. Baba anaunda

**Onesha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi zifuatazo:-**

70. Nilimuona Juma nilipofika Mbeya.
71. Ng'ombe aliyepita ameumia mguu.
72. Kule alikokwenda jana kulikuwa na bidhaa nyingi.
73. Kijana ambaye alitusimulia habari zake juzi amepata zawadi ya bahati nasibu ya Taifa.

**Tunga kirai kitenzi chenye muundo ufuatao:-**

74. Kitenzi+Kirai kiunganishi
75. Kitenzi+Nomino
76. Kitenzi+Nomino+Kitenzi
77. Kitenzi kishirikishi+Kivumishi+Kielezi
78. Kitenzi Kishirikishi+Nomino+kivumishi
79. Eleza maana ya vitenzi
80. Taja aina kuu za vitenzi

**Vibadilishe vitenzi vifuatavyo viwe katika kauli ya kutenda.**

81. Badili
82. Kata
83. Komboa
84. Zuia
85. Fika
86. Zoa
87. Jenga
88. Remba

89. Tumia
90. Lima.

**Bainisha mzizi wa asili kwa kila neno katika maneno yafuatayo:**

91. Anawaandikisha
92. Mkimbizi
93. Mlaji
94. Muumbaji
95. Nisingelipenda
96. Kuburudika
97. Sadifu
98. Aliokota
99. Walichopoka
100. Kipaumbele